LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA MTOTO

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA MTOTO

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


1. **Maana ya Mtoto ........ 11**
2. **Maslahi Bora ya Mtoto ........ 11**
3. **Haki za Mtoto ........ 11**
    - 3.1.Haki Wanazostahili Watoto ........ 11
    - 3.2.Haki ya Kuishi na Kuheshimiwa ........ 12
    - 3.3.Haki ya Kutokubaguliwa ........ 12
    - 3.4.Haki ya Kupata Jina, Utaifa na Kuwafahamu Wazazi Wake ........ 12
    - 3.5.Haki ya Kutoa Mawazo ........ 12
    - 3.6.Ulinzi dhidi ya Mateso na Udhalilishaji ........ 13
    - 3.7.Haki za Watoto wenye Ulemavu ........ 13
    - 3.8.Haki ya Kurithi ........ 14
    - 3.9.Haki ya Ulinzi wa Watoto dhidi ya Ukeketaji ........ 14
4. **Wajibu wa Mzazi ........ 15**
    - 4.1.Wajibu wa Mzazi au Mlezi Kutunza Mtoto ........ 15
    - 4.2.Wajibu wa Mzazi au Mlezi kulinda Haki za Mtoto ........ 16
5. **Wajibu wa Jamii ........ 17**
6. **Wajibu wa Serikali Kulinda Haki za Mtoto ........ 17**
    - 6.1.Wajibu wa Kulinda Watoto Waishio katika Mazingira Hatarishi ........ 18
    - 6.2.Wajibu wa Serikali za Mitaa Kuhakikisha kwamba Wazazi au Walezi Wanatimiza Wajibu wa Kulea na Kutunza Watoto ........ 19

**7. Ajira kwa Watoto** .......... **20**

**ANGALIZO** .......... **20**

**8. Mtoto anayestahili Uangalizi wa Vyombo Vingine** .......... **22**

**9. Ulinzi kwa Mtoto** .......... **24**

9.1.Ulinzi Mtoto Anaostahili .......... 24

9.2.Uuzaji wa Vileo kwa Mtoto .......... 24

9.3.Jukumu la Ulinzi .......... 25

9.4.Umuhimu wa Mtoto Kuwa Chini ya Uangalizi .......... 27

9.5.Kuisha kwa Muda wa Uangalizi .......... 28

**10. Mahakama ya Watoto** .......... **28**

10.1.Utaratibu wa Kuendesha Mashauri ya Watoto .......... 30

10.2.Wanaoruhusiwa Kuwepo wakati wa Uendeshaji Mashauri ya Watoto .......... 31

10.3.Dhamana .......... 32

10.4.Mtoto Anapopatikana na Hatia .......... 32

**11. Hitimisho** .......... **34**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma yakusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi

wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

# UTANGULIZI

Kwa muda mrefu kulikuwa na mkanganyiko juu ya tafsiri sahihi ya mtoto hapa Tanzania. Kulikuwa na sheria mbalimbali zilizotafsiri mtoto kwa njia tofauti hivyo kusababisha mtoto kunyimwa haki zake za msingi kisheria. Kutokana na hali hiyo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ilitungwa na Bunge ili kuondoa utata uliokuwepo. Sheria hii ilifuta sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Kuasili, Sheria ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa, Sheria ya vituo vya kulelea watoto wadogo na Sheria ya watoto walioko kwenye mgogoro na sheria. Pia Sheria ya mtoto ya mwaka 2009 ilifanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali kama vile, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Elimu, Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini, Sheria ya Kanuni za Adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai.

Kwa kiasi kikubwa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 imesaidia kutambua na kulinda haki za mtoto.

# 1. MAANA YA MTOTO

Mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18).

# 2. MASLAHI BORA YA MTOTO

Maslahi bora ya mtoto ni mambo mazuri, mema, yenye kumlinda, kumwendeleza na kulinda utu wa mtoto ambayo mtoto anatakiwa ayapate, afanyiwe au yazingatiwe kwenye mambo yote yamhusuyo.

Maslahi bora ya mtoto yatapewa kipaumbele katika matendo, maamuzi na mambo yote yanayohusu mtoto na ambayo yanatekelezwa na watu binafsi, mamlaka, idara, taasisi, makampuni yanapokuwa yanatekeleza majukumu yao ya kila siku.

# 3. HAKI ZA MTOTO

### 3.1. Haki Wanazostahili Watoto

Watoto wanastahili kupata haki na uhuru sawa na watu wazima. Haki zenyewe zimeainishwa katika Sheria ya watoto kama ifuatavyo;-

### 3.2. Haki ya Kuishi na Kuheshimiwa

Mtoto ana haki ya kuishi, kuheshimiwa, kupumzika, kuwa na uhuru wa mawazo, kupata matibabu elimu na makazi bora kutoka kwa wazazi au walezi wake au taasisi yeyote ambayo inahusika na uangalizi wa mtoto.

### 3.3. Haki ya Kutokubaguliwa

Mtoto ana haki ya kutobaguliwa. Kwa hiyo mtu yeyote haruhusiwi kumbagua mtoto katika mtazamo wa kijinsia, kabila, umri, dini, lugha, maoni ya kisiasa, ulemavu, hali ya kiafya, mila, asili ya kikabila, hali ya kiuchumi, ukimbizi au hali yeyote ile.

### 3.4. Haki ya Kupata Jina, Utaifa na Kuwafahamu Wazazi Wake

Mtoto ana haki ya kupata jina, utaifa kuwafahamu wazazi wake waliomzaa na ndugu zake wa karibu. Na kwa hiyo, kila mzazi anawajibu wa kusajili kuzaliwa kwa mtoto kwa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

### 3.5. Haki ya Kutoa Mawazo

Mtoto ana haki ya kutoa mawazo au maoni yake. Hakuna mtu atakayemzuia mtoto mwenye

uwezo wa kutoa mawazo au maoni haki ya kutoa mawazo, kusililizwa na kushiriki katika maamuzi yanayoathiri maisha na maslahi yake kulingana na umri na uwezo wake wa uelewa.

### 3.6. Ulinzi dhidi ya Mateso na Udhalilishaji

Sheria inakataza mateso ya aina yeyote dhidi ya mtoto, kama vile kumfanyia vitendo vya kikatili, kumpa adhabu zisizo za kibinadamu au kumdhalilisha mtoto ikijumuisha mila na desturi zozote zenye madhara kwa mtoto kimwili au kiakili.

Mtoto hatakiwi kupea adhabu mbaya ya aina yeyote au ni kubwa kwa kiwango chake kulingana na umri wa mtoto, hali ya mtoto kimwili na kiakili; na adhabu haitakuwa stahili kwa mtoto iwapo kutokana na umri mdogo wa mtoto au kwa sababu nyingine hawezi kuelewa lengo la adhabu hiyo.

### 3.7. Haki za Watoto wenye Ulemavu

Mtoto mwenye ulemavu anastahili kupata huduma maalum ya matibabu na nafasi sawa ya elimu na mazoezi pale inapowezekana ili kumsaidia kufikia malengo yake ya maisha.

### 3.8. Haki ya Kurithi

Mtoto ana haki ya kurithi mali za wazazi wake. Haki ya kurithi inawahusu watoto wote waliozaliwa ndani ya ndoa, waliozaliwa nje ya ndoa na walioasiliwa ili mradi wametambulika kisheria kama vile walitambulishwa na marehemu kabla ya kifo chake, wana nyaraka zinazoonesha uhusiano wao na marehemu au wamethibitishwa kisheria juu ya uhalali wao kuwa ni watoto wa marehemu.

Mtoto ana haki ya kutumia kwa busara mali ya mzazi wake aliyefariki. Hakuna mtu atakayemzuia mtoto kutumia kwa busara mali ya mzazi wake aliyefariki.

### 3.9. Haki ya Ulinzi wa Watoto dhidi ya Ukeketaji

Hakuna mtu anayeruhusiwa kumfanyia mtoto wa kike ukeketaji. Mtu atakayekiuka masharti ya sheria atakuwa amefanya kosa la jinai. Ikiwa itathibitika mtuhumiwa wa vitendo vya ukeketaji hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

# 4. WAJIBU WA MZAZI

Chini ya Sheria ya Mtoto mzazi, mlezi, ndugu au mtu au taasisi yeyote inayomlea mtoto ina wajibu wa kumtunza mtoto.

### 4.1. Wajibu wa Mzazi au Mlezi Kutunza Mtoto

Ni wajibu wa mzazi, mlezi au mtu yeyote anayekaa na mtoto kumtunza mtoto kwa kumpatia mtoto haki na mahitaji yafuatayo;-

a. Chakula;
b. Makazi;
c. Mavazi;
d. Matibabu ikiwa ni pamoja na kupata chanjo;
e. Elimu na malezi;
f. Uhuru; na
g. Haki ya kucheza na kupumzika

Vilevile mtu yeyote haruhusiwi kwa makusudi kumzuia mtoto kupata elimu, chanjo, chakula, makazi, matibabu ya kiafya, au kumnyima mtoto kitu chochote kinachohitajika katika maendeleo na ustawi wake.

## 4.2. Wajibu wa Mzazi au Mlezi kulinda Haki za Mtoto

Kila mzazi ana kazi na wajibu, uwe wa kisheria, kisera, kimkakati, kimpango, kimalezi au vinginevyo kumwangalia mtoto wake, kwa kufanya yafuatayo;-

a. Kulinda mtoto dhidi ya kufanyika au kutekelezwa kwa vitendo vya, kibaguzi, unyanyasaji, kuishi katika mazingira hatarishi ya kiroho au kimwili;
b. Kutoa malezi, ulinzi, msaada na matunzo ya mtoto ili kuhakikisha ustawi na makuzi bora ya mtoto;
c. Kuhakikisha kuwa pale mzazi asipokuwepo basi mtoto yule awe chini ya uangalizi wa mtu mwenye uwezo wa kumlea;
d. Kutunza na kuhifadhi desturi mustakabali wa jamii na taifa; na
e. Kutunza na kuhifadhi mila sahihi za jamii na taifa lake kwa ujumla kama ilivyo kwa wanajamii na Watanzania wengine.

## 5. WAJIBU WA JAMII

Wajibu wa wanajamii wenyewe taarifa au ushahidi kuwa haki za mtoto zinavunjwa na mzazi, mlezi, ndugu au mtu yeyote katika jamii ambaye kwa wakati huo anamlea au mtoto yuko chini ya uangalizi wake kutoa taarifa ya unyanyasaji kwenye ofisi za Serikali za Mitaa au taasisi, idara au chombo chochote kinachoweza kumsaidia mtoto.

Mzazi, mlezi, ndugu au mtu yeyote katika jamii ambaye kwa wakati huo anamlea mtoto au mtoto yuko chini ya uangalizi wake atahesabika kuwa kavunja haki za mtoto ikiwa atapuuzia au kukataa kutoa chakula, makazi, matibabu, elimu, nguo au haki za mtoto kucheza na wenzake.

## 6. WAJIBU WA SERIKALI KULINDA HAKI ZA MTOTO

Serikali za Mitaa zitawajibika kulinda na kutetea maslahi ya mtoto ili kuhakikisha kuwa watoto

wanalelewa katika mzingira stahiki na kwa mujibu wa maadili ya jamii na taifa letu.

Afisa ustawi wa jamii kupitia Serikali za Mitaa anawajibu wa kutoa maelezo na mafunzo kwa wazazi, walezi, ndugu na jamii husika juu ya hatua na ustawi wa mtoto.

### 6.1. Wajibu wa Kulinda Watoto Waishio katika Mazingira Hatarishi

Serikali za Mitaa zote zinatakiwa kutunza daftari la usajili wa watoto wote yatima au watoto walio katika mazingira hatarishi kwa maeneo yao ya utawala ili kuhakikisha kwamba wanawawezesha watoto hao kukua na kujitegemea kama ilivyo kwa watoto wengine walio na wazazi au malezi.

Kadhalika, ni wajibu wa serikali za mitaa kuhakikisha kwamba watoto walio katika uhitaji au yatima wanapata mahali pa kuishi na kuendelea na shughuli zao, ustawi na maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwatafutia shule.

### 6.2. Wajibu wa Serikali za Mitaa Kuhakikisha kwamba Wazazi au Walezi Wanatimiza Wajibu wa Kulea na Kutunza Watoto

Kila Serikali ya Mtaa, kwa kushirikiana na jeshi la polisi, inatakiwa kufanya kila juhudi iwezekanavyo ili kuwatafuta na kuwapata wazazi, walezi au ndugu wa watoto waliotelekezwa kwa lengo la kuwarudisha watoto wale kwa wazazi au walezi wao au kwa jamii yao ili waweze kukua na kulelewa katika misingi ya maisha bora.

## 7. AJIRA KWA WATOTO

Mtoto mwenye umri wa kuanzia miaka 14 ana haki ya kufanya kazi nyepesi na kupata malipo stahiki.

### ANGALIZO

Ieleweke kuwa, kazi nyepesi ni zile ambazo haziathiri afya ya mtoto, hazikwamishi maendeleo yake kielimu au makuzi yake. Hii ni pamoja na kazi ambazo hazina madhara katika utendaji wa kazi za kimasomo zinazotolewa ili azifanye akiwa nyumbani, haki yake ya kucheza, au kazi ambazo haziathiri uhuru wake wa kushiriki katika mafunzo ya kijamii. Kazi hizo zinatakiwa kuzingatia umri na uelewa wa mtoto.

Kwa hali hiyo, mtu haruhusiwi kumwajiri mtoto katika kazi yeyote ile ya kinyonyaji.
Pia sheria inasisitiza kuwa, mtu haruhusiwi kumwajiri mtoto katika kazi yeyote ambayo ni hatari katika afya yake, elimu, akili, maumbile na hata katika maendeleo yake ya kiroho.

**Kazi yeyote itahesabiwa kuwa ya kinyonyaji endapo kazi hiyo itakuwa na viashiria au mambo yafuatayo:-**

a. Inaathiri afya na makuzi ya mtoto;
b. Inazidi masaa sita kwa siku;
c. Hailingani au inazidi umri wake;
d. Inamlipa mtoto malipo kidogo na yasiyostahili; au
e. Kazi hiyo inamhitaji mtoto kufanya kazi nyakati za usiku ambazo huanza muda wowote kati ya saa mbili za usiku hadi saa kumi na mbili za asubuhi.

**Sheria pia inaainisha kazi hatarishi kwa mtoto kama ifuatavyo:-**

a. Zinazomfanya au kumlazimisha mtoto aingie baharini;
b. Zinazomfanya mtoto au kumlazimisha mtoto aingie mgodini au kwenye machimbo ya mawe;
c. Zinazomfanya au kumlazimisha mtoto kuponda mawe;
d. Zinazomwingiza au kumlazimisha aingie katika viwanda ambavyo madawa huzalishwa au kutumika;

e. Zinazotumia mashine mbalimbali;

f. Kazi za baa, vilabu vya pombe, hoteli, na mahali pengine popote pa starehe; na

g. Kazi ambazo zinamweka mtoto katika mazingira ya jinsia ya mahusiano ya kingono au ukahaba bila kujali kama analipwa au halipwi.

Hivyo basi, kila mwajiri ambaye ameajiri mtoto/ watoto, anatakiwa kuhakikisha kwamba kila mtoto aliyeajiriwa kihalali anapewa ulinzi dhidi ya mazingira yeyote ya unyanyasaji au vitendo vyovyote vinavyoweza kumwathiri kulingana na umri wake au uwezo wake wa kufanya kazi.

## 8. MTOTO ANAYESTAHILI UANGALIZI WA VYOMBO VINGINE

**Mtoto mwenye mahitaji ya uangalizi ni Yule:-**

a. Aliye yatima na aliyetelekezwa na wazazi wake;

b. Aliyenyanyaswa na walezi wake;

c. Aliye na wazazi au walezi wake lakini hawatekelezi wajibu wao;

d. Asiye na mahali pa kwenda;

e. Anayelelewa na mzazi au mlezi ambaye kwa sababu alitenda makosa ya jinai, au ni mlevi, hafai kulea mtoto;

f. Anayerandaranda mitaani na ambaye hana mahali pa kuishi;

g. Anayeishi kwa kuombaomba;

h. Anayelelewa na mtu maskini;

i. Anayekaa na mtenda makosa ya jinai (mhalifu) au malaya;

j. Anayekaa kwenye nyumba au anaishi kwenye mazingira ambayo hutumiwa na malaya;

k. Anayekaa na mtu ambaye alishatenda au anaweza kutenda kosa la kusafirisha watoto kinyume cha sheria (Usafirishaji haramu wa Watoto);

l. Mtoto huyo anayehisiwa kuwa si mwadilifu;

m. Ana umri chini ya miaka 12;

n. Anayeweza kuingiwa na vishawishi visivyo vya kiadilifu;

o. Anayeishi na mtu mwenye ulemavu ambaye ulemavu wake ni kikwazo katika malezi bora ya mtoto; au

p. Anayeishi katika mazingira yeyote ambayo yanaweza kuonekana si salama mbele ya kamishina wa Ustawi wa Jamii

# 9. ULINZI KWA MTOTO

## 9.1. Ulinzi Mtoto Anaostahili

Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kumfanyia mtoto ukatili au vitendo vya kinyama, adhabu zinazokiuka utu au kumdhalilisha ikiwa ni pamoja na mila na desturi zinazodhalilisha na zinazoumiza mwili na akili ya mtoto na maendeleo yake ya kiroho.

Mmiliki au mpangaji anayeendesha biashara ya disko, baa au klabu za usiku hatakiwi kumruhusu mtoto kuingia ndani ya jengo hilo au sehemu ya biashara hiyo.

## 9.2. Uuzaji wa Vileo kwa Mtoto

Marufuku kuuza sigara, pombe, madawa ya kulevya, vileo au mvinyo wowote kwa mtoto. Na mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda makosa hayo atapewa adhabu kali.

### 9.3. Jukumu la Ulinzi

Afisa wa Ustawi wa Jamii atakapoona mtoto anateswa, ananyanyaswa na wazazi wake, walezi wake au mtu yeyote mwenye wajibu wa kumwangalia mtoto anaweza kupeleka maombi maalum mahakamani kuomba mahakama itoe amri ya uangalizi wa mtoto asiteswe au kunyanyaswa kwa kipindi cha mwaka mmoja au mpaka pale atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane (18).

Afisa Ustawi wa Jamii au mtu yeyote anayefaa au ndugu anaweza kupewa jukumu au amri ya kumwangalia mtoto asiteswe. Inaweza kuwa katika jamii wakati mtoto atabakia kuwa mikononi mwa wazazi wake au walezi wake.

Vivyo hivyo, Afisa Ustawi wa Jamii anaweza kupeleka maombi maalumu mahakamani kuomba mahakama itoe amri ya kumtoa mtoto nyumbani kwa wazazi wake au kwa walezi wake wanaomtesa, kumnyanyasa au

aliye katika mazingira yanayopelekea kumtesa na kumnyanyasa kwa kipindi cha miaka mitatu au mpaka pale mtoto atakapofikisha umri wa miaka 18 ili mtoto yule apelekwe mahali ambapo atapata matunzo safi na salama kwa maslahi yake kwa muda huo.

Hali kadhalika, Afisa wa Ustawi wa Jamii anaweza kumjumuisha katika maombi yake mahakamani au katika mahakama, au mahakama inaweza kuongea katika amri yake, amri ya kumlazimisha mzazi au mlezi kulipa gharama za matunzo ya mtoto atakapokuwa ameondolewa mikononi mwao.

Baada ya Afisa wa Ustawi wa Jamii kufanikiwa kumuondoa mtoto katika mazingira hatarishi, atatafuta mahali salama pa kumlea na kumtunza mtoto kwa kuzingatia maslahi yake. Mahali hapo panaweza kuwa;-

a. Makazi ya watoto yaliyothibitishwa na mamlaka husika,
b. Kwa mtu ambaye anafaa mwenye

kuaminika;

c. Kwa mzazi, mlezi anayefaa kama ilivyo katika taratibu za ulezi wa watoto chini ya sheria ya mtoto; au

d. Nyumbani kwa babu au bibi wa mtoto, walezi ndugu au jamaa zake wa karibu wenye mwenendo mzuri wa kumsaidia mtoto.

### 9.4. Umuhimu wa Mtoto Kuwa Chini ya Uangalizi

Kama ilivyowekwa bayana na Sheria ya Mtoto, amri ya uangalizi wa mtoto anayeteswa na kunyanyaswa imewekwa kwa sababu zifuatazo;-

a. Kumwondoa mtoto katika mazingira ambayo anapata shida au yanapelekea kupata shida;

b. Kumsaidia mtoto aishi maisha salama na kuwasaidia wale walioshindwa kumlea vizuri wapate mafunzo mazuri ya malezi;

c. Kupata nafasi ya kuangalia mazingira yaliyopelekea kupata amri ya kumtoa mtoto ili kuchukua hatua za kutatua tatizo na kubaini chanzo cha tatizo hilo

na kumwezesha mtoto arudi katika jamii aliyokuwa anaishi.

### 9.5. Kuisha kwa Muda wa Uangalizi

Amri ya uangalizi wa mtoto inaweza kuondolewa na Mahakama kwa kuzingatia maslahi ya mtoto baada ya watu au idara zifuatazo kufanya maombi mahakamani;-

a. Mtoto kupatiwa mdhamini au mwangalizi wake;
b. Afisa Ustawi wa Jamii;
c. Afisa wa Polisi;
d. Mzazi, mlezi au ndugu wa motto; au
e. Mtu yeyote mwenye jukumu la uzazi.

## 10. MAHAKAMA YA WATOTO

Sheria ya Mtoto inaanzisha Mahakama ya Watoto ikiwa ni pamoja na kutoa utaratibu wa uendeshaji wa Mahakama hiyo. Mahakama hii itajulikana kama Mahakama ya Watoto kwa ajili ya kusikiliza na kuamua mashauri yote yanayohusu watoto.

Ili kuhakikisha kuwepo kwa mahali pa kuendeshea mashauri ya watoto, Mheshimiwa Jaji Mkuu kupitia Gazeti la Serikali atatenga au kutangaza namna au jinsi Mahakama ya Mtoto inaweza kuanzishwa kimiundo mbinu au kiutaratibu katika maeneo yaliyokuwa yanatumika na Mahakama za Mwanzo na kuzifanya kuwa Mahakama za Watoto.

**Mahakama ya watoto itakuwa na kazi ya kusikiliza mashauri yafuatayo;-**

a. Mashauri ya jinai dhidi ya mtoto,
b. Maombi yanayohusu matunzo ya mtoto.
c. Maombi yanayohusu uhalali wa mzazi/wazazi.

Pamoja na mashauri tajwa hapo juu, Mahakama ya Watoto itakuwa na uwezo wa kusikiliza mashauri mengine kama itakavyoagizwa na sheria zingine. Sheria ya Mtoto inasisitiza kuwa mashauri yahusuyo watoto yasikilizwe katika maeneo tofauti na maeneo yanayotumika kusikiliza mashauri ya watu wazima.

### 10.1. Utaratibu wa Kuendesha Mashauri ya Watoto

Utaratibu wa kuendesha mashauri ya watoto utatolewa na Jaji Mkuu wa Tanzania. Hata hivyo, utaratibu huo utazingatia mambo yafuatayo;-

a. Kuhakikisha kuwa Mahakama ya Watoto inakaa mara kwa mara.

b. Mashauri ya watoto kundeshwa kwa siri, mbele ya wahusika pekee.

c. Mashauri ya watoto yataendeshwa kwa njia rahisi isiyo rasmi, yaani isiyofungwa sana na taratibu za kisheria. Ikiwa ni pamoja na kutumia njia ya uchunguzi ili kumwepusha mtoto kuwa katika mazingira ya ushindani wa kisheria.

d. Uwepo wa Afisa Ustawi wa Jamii unahitajika katika mashauri yote yamhusuyo mtoto.

e. Kuwepo kwa haki ya kuwepo kwa mzazi, mlezi au mwangalizi wa mtoto.

f. Mtoto atakuwa na haki ya kuwakilishwa na wakili pale anapopatikana au kuwezekana.

g. Mtoto ataarifiwa juu ya haki yake ya kukata rufaa; na

h. Mtoto atakuwa na haki ya kutoa maelezo na mawazo ya shauri lake kama maelezo ya utetezi, ushahidi n.k.

Shauri la mtoto isipokuwa shauri la mauaji litasikilizwa mara moja kwa muda wa siku moja na kutolewa uamuzi siku hiyo hiyo au ndani ya muda muafaka ambao utazingatia maslahi ya mtoto

### 10.2. Wanaoruhusiwa Kuwepo wakati wa Uendeshaji Mashauri ya Watoto

Watu wafuatao wanaweza kuruhusiwa na **Mahakama ya Watoto kuwepo katika shauri la mtoto**:-

a. Wahusika wakuu katika shauri mfano, mawakili, mashahidi na watu wengine ambao wanahusika moja kwa moja na shauri la mtoto;

b. Mtu yeyote ambaye mahakama itamruhusu kuwepo wakati wa shauri.

### 10.3. Dhamana

Mara tu mtoto atakapokuwa mikononi kwa polisi, ni budi kumpeleka mahakamani mara moja bila kuchelewa na baada ya hapo, Afisa wa Polisi aliyepewa jukumu hilo atamruhusu kuwa nje ya mahabusu kwa udhamini wa mzazi wake, mlezi ndugu au bila dhamana yeyote, isipokuwa tu pale ambapo ni kosa la mauaji, kuna mazingira hatarishi au pale afisa huyo anapokuwa na ushahidi kuwa kuna mazingira hatarishi dhidi ya mtoto.

Kama mtoto atakosa dhamana kutokana na mazingira tajwa hapo juu, basi afisa polisi atafanya kila awezalo kumtenganisha mtoto na mahabusu ya watu wazima.

### 10.4. Mtoto Anapopatikana na Hatia

Sheria ya Mtoto inazuia mtoto kufungwa kifungo chochote kama vile vifungo vya watu wazima. Badala yake mtoto anaweza kupewa adhabu ambazo zimetajwa katika sheria.

Sheria inatoa aina ya adhabu na matunzo kwa ajili ya kumrekebisha mtoto na kumrudisha katika mazingira ya uadilifu kama watoto wengine waadilifu.

**Zifuatazo in aina ya adhabu au kemeo kwa mtoto;-**

a. Kupewa muda maalum wa kujirudi kupitia uangalizi wa mzazi, mlezi, ndugu, Afisa Ustawi wa Jamii au mtoto yeyote aliyeamriwa kufanya hivyo na mahakama;
b. Kulipa faini, fidia au gharama kwa kupitia kwa mzazi, mlezi au ndugu;
c. Kupelekwa katika shule maalumu katika kipindi maalumu kwa ajili ya matunzo.

# 11. HITIMISHO

Sheria hii ya Watoto imejaribu kuunganisha sheria zote za Tanzania zinazogusa maslahi ya mtoto kwa njia moja au nyingine. Pia sheria hii imezingatia kwa kiasi kikubwa miongozo na misingi iliyowekwa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*